

## **MHANDO WA TBC KIZIMBANI KWA UHUJUMU UCHUMI**

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Tido Mhando, amefikishwa kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dares Salaam, akikabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi likiwemo moja la kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Shilingi milioni 887 wakati akiwa TBC.

Tido, ambaye kwa saswa ni Mkurugenzi wa Azam Media Ltd, alisomewa mashtaka na waendedsha mashtaka wa TAKUKURU Leonard Swai, Pendo Temu na Aneth Mavika, Januari 25, 2018 mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Victoria Nongwa.

Katika shtaka la kwanza hadi la nne, upande wa mashtaka uliiambia mahakama kuwa Tido alitenda makosa manne ya matumizi mabaya ya madaraka na moja la kuisababishia serikali hasara kubwa kati ya Juni 16, 2008 na Novemba 16, 2008, akiwa mwajiriwa wa TBC kwa nafasi ya Mkuirugenzi Mtendaji, akiwa Dubai, Falme za Kiarabu.

Waendesha mashtaka waliambia mahakama kuwa katika kipindi hicho mshtakiwa akiwa Mkurugenzi Mtendaji wa TBC kwa makusudi alikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 21 ya mwaka 2004 kwa kuingia mikataba minne inayohusiana na shughuli za TBC katika utangazaji, kwa kusaini makubaliano kati ya TBC na Channel 2 Group Corporation (BVI) ya Dubai, bila kutangaza zabuni kama inavyotakiwa na sheria hii.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Juni 16, 2008 mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa TBC kwa nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji, akiwa Dubai, Falme za Kiarabu katika utekelezaji wa majukumu yake aliingia mkataba wa ubia wa uendeshaji na urushaji program za matangazo, kwa kusaini makubaliano kati ya TBC na Channel 2 Group Corporation (BVI), bila kutangaza zabuni kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi ya umma hivyo kuinufaisha BVI.

Juni 20, 2008, mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa TBC kwa nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji, akiwa Dubai, Falme za Kiarabu, katika utekelezaji wa majukumu yake aliingia mkataba wa urushaji wa matangazo kwa njia ya kidigitali (Digital Terrestrial Broadcasting - DTTV), kwa kusaini makubaliano kati ya TBC na BVI, bila kutangaza zabuni kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi ya umma hivyo kuinufaisha BVI.

Agosti 4 na 11, 2008 Tido akiwa mwajiriwa wa TBC kwa nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji, akiwa Dubai, Falme za Kiarabu katika utekelezaji wa majukumu yake aliingia mkataba mwingine wa nyongeza wa kununua, kusambaza, kusimika vifaa vya kurushia matangazo ya televisheni na minara, kwa kusaini makubaliano kati ya TBC na BVI, bila kutangaza zabuni kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi ya umma, hivyo kuinufaisha BVI.

Novemba 16, 2008 pia, mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa TBC kwa nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji, akiwa Dubai, Falme za Kiarabu, katika utekelezaji wa majukumu yake, aliingia mkataba mwingine wa nyongeza wa uendeshaji wa miundombinu ya utangazaji ya kidigitali

(Digital Terrestrial Broadcasting - DTTV), kwa kusaini makubaliano kati ya TBCna BVI, bila kutangaza zabuni kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi ya umma na hivyo kuinufaisha BVI.

Upande wa mashtaka uliambia mahakama pia kuwa kati ya Juni 16, 2008 na Novemba 16, 2008, Tido akiwa mwajiriwa wa TBC kwa nafasi ya Mkuirugenzi Mtendaji, akiwa Dubai, Falme za Kiarabu, katika utekelezaji wa majukumu yake aliisababishia serikali hasara ya Shilingi 887,122, 219.19.

Mshtakiwa aliyekuwa akitetewa na wakili wa kujitegemea, Ramadhan Maleta, alikana mashtaka dhidi yake na upande wa mashtaka uliambia mahakama kuwa uko tayari kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali kwa tarehe itakayo pangwa na mahakama.

Masharti ya dhamana yaliyotolewa na mahakama ni mshtakiwa kuweka fedha taslimu kiasi cha Shilingi milioni 444 au kuweka dhamana ya mali zisizohamishika zenye thamani hiyo ya fedha pamoja na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa umma. Pia mahakama ilimtaka mshtakiwa kutosafiri nje ya mkoa bila kibali chake.

Mshtakiwa alidhaminiwa baada ya kutimiza masharti ya dhamana na kesi imeahirishwa hadi Februari 23 mwaka huu itakapokuja kwa ajili ya kutajwa.



Tido Mhando( kushoto) akiwa mahakamani akisubiri kusomewa mashtaka yake